# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA NANE

**04 FEBRUARI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 04 FEBRUARI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (Mapitio ya Nusu Mwaka 2015/2016) [*Monetary Policy Statement (The Mid – year Review 2015/2016)*]

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**92. MHESHIMIWA RIZIKI SHAHARI MNGWALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na tatizo sugu nchini kwa baadhi ya vituo vya afya na zahanati za Serikali kuwa na watumishi wasio na sifa za utabibu:-

Je, Serikali inatumia vigezo gani kuwapeleka watumishi wasio na sifa katika zahanati na vituo vya afya.

## OFISI YA MAKAMU WA RAIS:

**93. MHESHIMIWA ALI HASSAN KING (JANG'OMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais:- Tatizo la mazingira ni tatizo mtambuka na tumeona jinsi Serikali ilivyojipanga kutatua tatizo hili kwenye maeneo tofauti:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo la Mazingira linalojitokeza la kudidimia kwa Ardhi kwenye makazi ya watu.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**94. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Kazi ya vikosi vya ulinzi na usalama ni kulinda raia na mali zao pamoja na kulinda mipaka ya nchi; lakini baadhi yao wamekuwa wakienda kinyume na sheria kama vile kuwapiga na kuwasababishia wananchi ulemavu au vifo:-

(a) Je, mpaka sasa ni askari wangapi wameshachukuliwa hatua;

(b) Je, ni askari wangapi mpaka sasa wamekutwa na hatia na kufukuzwa kazi.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**95. MHESHIMIWA JUMA SELEMANI NKAMIA (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua mashine mpya ya CT-Scan kwa ajili ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

**96. MHESHIMIWA FATUMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-
Ujenzi wa Maternity Complex katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma ulianza tangu mwaka 2009 ambapo majengo hayo yana uwezo wa kuweka vitanda 180, lakini hadi leo hii jengo hilo halijakamilika kutokana na Serikali kuamua kuimarisha huduma ya afya ya mama na mtoto kwa kuzingatia vipaumbele vya tekeleza kwa matokeo makubwa sasa (BRN):-

Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kutekeleza matokeo makubwa sasa kwa kuiangalia hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma kwa jicho la pekee kwa kuipatia fedha ili

jengo hilo likamilike haraka kuwaondolea adha kubwa wanayopata kina mama wakati wa uzazi.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**97. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Serikali kupitia Benki ya Dunia ilianzisha mradi wa maji katika Miji ya Hydom, Masieda, Tumati Arri na Bwawa la Dongobeshi lakini mpaka sasa mradi huo haujakamilika baada ya fedha kusitishwa:-

Je, Serikali imejipangaje kumalizia miradi hiyo ili wananchi wapate maji.

**98. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Tatizo la maji limeendelea kuwa kubwa Morogoro Mjini pamoja na Mji Mdogo wa Gairo ambapo wanawake wanapata shida sana kutafuta maji:-

Je, ni lini tatizo hilo la maji litaisha.

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**99. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wavuvi kutoka Ukanda wa uvuvi wa kisiwa cha Unguja na wale wa ukanda wa Mkoa

wa Dar es Salaam na Pwani wamekuwa wakifanya uvuvi kwenye maeneo yanayoingiliana, lakini hivi punde wavuvi wa Unguja wameanza kusumbuliwa na kuwekewa vikwazo vya kuvua maeneo ya Tanzania Bara:-

(a) Je, kwa nini wavuvi hao wasumbuliwe na kuwekewa vikwazo;

(b) Je, wavuvi hao hawana haki ya kuvua maeneo hayo;

(c) Je, ni kwa nini Serikali isiwaelimishe juu ya wanachotakiwa kufanya au wasichotakiwa kufanya.

**100. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Mnada wa Magena Wilayani Tarime ulifungwa na kusababisha adha kubwa kwa Halmashauri ya mji wa Tarime kupoteza mapato ya ushuru wa mifugo inayouzwa Nchi jirani ya Kenya, Sambamba na ukosefu wa ajira kwa wakazi wa Tarime:-

Je, mnada huo wa Magena utafunguliwa lini ili kutoa fursa za ajira na kuokoa mapato mengi yanayopotea kwa sasa.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

**101. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali imeweka mpango wa umeme vijijini ambapo kwa Jimbo la Magu ni asilimia 20 tu ya vijiji ndivo vimepata umeme ambalo ni hitaji muhimu kwa kila Mtanzania:-

(a) Je, asilimia 80 ya vijiji vilivyobaki vitapata lini umeme;

(b) Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na tatizo la kukatika katika kwa umeme nchini.

## III. KAMATI YA MIPANGO:

**(Majadiliano yanaendelea)**

**DODOMA DKT. T. D. KASHILILAH**
**04 FEBRUARI, 2016 KATIBU WA BUNGE**